MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu

# Dhima za Wahusika Jumui katika Riwaya za Kiswahili za Kimajaribio

Joyce Obetch*, James Ontieri, Mark Odawo

*Idara ya Isimu Na Lugha, Chuo Kikuu cha Rongo, Kenya*

**IKISIRI**

Waandishi wa kazi za fasihi huwasawiri wahusika kwa uangalifu mkubwa ili kuwaweka katika nafasi za kutekeleza majukumu anuai kisanaa na hivyo kuwapa dhima maalum. Ni kutokana na mtagusano na maingiliano ya wahusika katika mazingira maalum ambapo mitazamo na tasnifu ya watunzi hudhihirika. Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu usawiri wa wahusika katika tungo anuwai za kisanaa. Hata hivyo, dhima za wahusika jumui katika riwaya za kimajaribio za Kiswahili hazijashughulikiwa kikamilifu. Kwa mujibu wa hoja hii, makala haya yanajadili jinsi usawiri wa wahusika jumui katika riwaya teule za kimajaribio za Babu Alipofufuka (Mohamed, 2001) na Dunia Yao (Mohamed, 2006) unavyowasilisha dhima zao kihalisia. Nadharia ya Uhalisiamazingaombwe iliyoasisiwa na Roh (1925) imetumika katika kuchanganua data kwa lengo la kutimiza mahitaji ya utafiti huu. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa riwaya teule, kisha zikachanganuliwa na kuwasilishwa kimaelezo. Utafiti umebaini kuwa wahusika jumui wametumiwa kama kielelezo cha maporomoko ya jamii, kielelezo cha ukengeushi, kielelezo cha umma uliodhulumiwa, kielelezo cha viongozi wabinafsi na wafisadi, zana ya kutekelezea umazingaombwe, kielelezo cha viongozi wenye mapuuza na kama zana ya kutekelezea hukumu. Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kuwa amilifu katika kutoa welewa wa wahusika jumui katika fasihi ya kimajaribio ya Kiswahili.

**KUHUSU MAKALA**

*Maneno Muhimu:*
Dhima,
Wahusika Jumui,
Riwaya za kimajaribio

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 16 Agosti 2025
Tarehe ya Kurekebishwa: 15 Septemba 2025
Tarehe ya Kukubalika: 20 Septemba 2025
Mtandaoni: 3 Oktoba 2025

## 1. Utangulizi

Waandishi wa kazi za fasihi huwatumia wahusika wa aina tofauti katika kazi zao lakini wahusika jumui hawajashughulikiwa sana katika tafiti za kitaaluma. Jinsi ambavyo wahusika jumui wanavyotumiwa katika riwaya nyingi za kimajaribio hausababishi kuwepo kwa mshikamano wala muumano wa hadithi toka mwanzo hadi mwisho. Jambo hili limewatatiza wasomaji katika kubainisha ujumbe unaowasilishwa na waandishi wa riwaya hizo. Kazi hizo za kimajaribio zinahitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina ili kubainisha sababu za kuwatumia wahusika jumui katika masimulizi na matukio yanayosukwa na waandishi. Kuna tofauti kubwa kati ya mambo ya kweli katika dunia halisi na yale ya kindoto katika fasihi za kimajaribio. Hili ni dhihirisho kuwa kuna pengo kati ya mambo tunayoyajua katika uhalisi na yale ambayo hatuyaelewi katika ndoto, japo yanaonekana kana kwamba ni matukio halisi. Hivyo ndivyo tunavyowajua wahusika katika riwaya nyingi ambapo yale yanayotendwa na wahusika wa kijadi na waliowasilishwa katika mkondo wa kihalisia huwa wanashabihi hali zetu za kila siku katika jamii. Matumizi ya wahusika na uhusika yasioweza kuyumkinika katika riwaya teule za Dunia Yao (Mohamed, 2006) na Babu Alipofufuka (Mohamed, 2001) na sababu za kutumika kwake ni jambo lisiloeleweka wazi. Utafiti huu, hivyo basi ulichunguza dhima za wahusika jumui katika uwasilishaji wa maudhui katika riwaya teule za kimajaribio za Kiswahili.

Kwa mujibu wa Lee (2004), mhusika jumui ni yule anayeundwa na watu wawili au zaidi wa maisha halisi, watu wa kubuni au wasio wa kubuni. Wamitila (2010) anaongeza kuwa sifa ya ujumui wa wahusika inalenga kuakisi ugumu uliopo katika kuiweka mipaka ya wazi katika utunafsi wa wahusika. Kwa msingi huo, anasema kuwa mhusika huyu anawasilishwa kwenye misingi ya falsafa au itikadi fulani na hivyo kuweza kuelezwa kama ‘mhusika wa kiitikadi’ au ‘mhusika wa kifalsafa’ Wahusika hutekeleza dhima mbalimbali katika kazi za fasihi. Kwa mujibu wa Wamitila (2003) dhima ni istilahi inayotumiwa kurejelea kazi ya mhusika katika tanzu za fasihi. Dhima za wahusika hudhihirika wanapotagusana na kuingiliana na wahusika wengine katika mandhari anuwai. Hali ya kimajaribio hutoa sura iliyozoeleka na kuweka sura mpya ambayo si ya kawaida. Mulokozi (1996) na Wamitila (2003) wanasema kuwa riwaya ya kimajaribio ni ile inayoujadili mkondo wa nafasi ya riwaya iliyotungwa bila kuzingatia kanuni za kawaida za uandishi. Wanasema kuwa aina hii ya riwaya hutosheleza mahitaji ya karne ya 21 katika kuwakilisha ukweli wa

*Mwandishi Mkuu. Simu: +254726269351; Barua Pepe: jobetch@gmail.com

Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.
Nukuu: Joyce O., James O., & Mark O. (2025). Dhima za Wahusika Jumui katika Riwaya za Kiswahili za Kimajaribio. Jarida la Kiswahili Sanifu 2(2), 11 – 18.

© 2025 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

maisha. Ni katika msingi huu ambapo riwaya za Dunia Yao (Mohamed, 2006) na Babu Alipofufuka (Mohamed, 2001) ziliteuliwa ili kuchunguzwa kama riwaya za kimajaribio. Makala hii inaangazia dhima za wahusika jumui katika riwaya za kimajaribio za Said Ahmed Mohammed.

## 2. Riwaya za Babu Alipofufuka na Dunia Yao

Babu Alipofufuka (Mohamed, 2001) na Dunia yao (Mohamed, 2006) ni riwaya za Kimajaribio. Kazi hizi zimedhihirisha mabadiliko makubwa katika mkabala na mkondo wa kisanii kwa kukiuka kaida zilizozoeleka za uandishi na hivyo kujikita katika umajaribio. Mohamed alijitahidi kubuni riwaya za Kiswahili katika usasabaadaye kwa kuchanganya mitindo ya kiuhalisia na kiuhalisiajabu, ili kupinga ukoloni mamboleo na utandawazi kutokana na matatizo ya ndani kwa ndani na pia kutokana na kani zinazotoka nje katika mtazamo wa Afrika Mashariki. Kimaudhui, riwaya hizi zimeshughulikia matatizo yanayoikabili dunia ya leo, hasa ya kiutandawazi. Kulingana na Mohamed, utandawazi ni tatizo kubwa na sugu kabisa. Kwa kiwango fulani, matatizo ya ndani ya nchi na jamii husika yameshughulikiwa. Hivyo basi, kwa kiasi kikubwa riwaya hizi zimekiuka mipaka ya kitaifa na kieneo.

### 2.2. Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhalisiamazingaombwe ambayo kwa mujibu wa Zamora (1995), iliasisiwa mwaka wa 1925 na mjerumani Franz Roh. Kwa sababu alikuwa mhakiki wa sanaa, alitumia istilahi uhalisiamazingaombwe katika muktadha wa sanaa kuelezea jinsi ya kusawiri aina fulani ya muujiza uliomo kwenye uhalisi uliozoelewa na unaotokana na ujarabati. Hata hivyo, kulingana na Warnes (2006), matumizi ya awali kabisa ya istilahi 'uhalisiamazingaombwe' yanapatikana katika maandishi ya mshairi Friedrich Freiherr von Hardenberg, maarufu kwa lakabu ya kishairi Novalis, aliyezaliwa mwaka wa 1772 na kufariki mnamo mwaka wa 1801. Warnes (2006) anadai kuwa Novalis hakuikuza mno dhana ya uhalisiamazingaombwe hata ingawa alikuwa wa kwanza kuitumia. Green (2009) naye anasema kuwa, Novalis (1772-1801) alihusika katika kubuni istilahi ya uhalisia mazingaombwe naye Roh (1925) alichangia katika kuijenga dhana ya uhalisia mazingaombwe.

Roh (1925) anasema kuwa, Uhalisiamazingaombwe ni uwasilishi wa ujumbe unaofichua hali ya kiroho na uajabu katika chombo kwa kubainisha, kudhihirika kwake na kukifanya zaidi ya kuwa halisi. Katika hali hii, uhalisiamazingaombwe hutuingiza katika ulimwengu wa kinjozi kwa kuwasilishwa kama “uhalisi.” Hivyo, unafuta mipaka kati ya uhalisia na udhahania na huchanganya masuala ya kihalisia na yale ya kiajabuajabu. Mambo yanayumbishwayumbishwa baina ya ulimwengu wa kihalisia na ule wa kufikirika au wa kimiujizamiujiza.

Cooper (1998), Mbatia (2002) na Wamitila (2003), wanaafikiana kuwa uhalisiamazingaombwe ni mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa kiuhalisia, kwa kuyaeleza moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Matukio ya kiajabu, ya kichawi, yasiyoaminika, ya kushangaza na kuogofya huwasilishwa kwa namna inayoyafanya yaonekane ya kawaida. Mtindo huu hutumika kuonesha kuwa matukio ya kifantasia hupatikana katika maisha ya kawaida ya jamii. Uchanganuzi wa data za utafiti huu uliongozwa na mhimili kuwa ‘wahusika huathiriwa na nguvu ambazo hawaelewi wala kuweza kuzidhibiti; yaani nguvu ambazo zinazidi nguvu za wanadamu wa kawaida. Hivyo hawana msukumo wa kujinasua’

## 3. Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulitumia mbinu ya kipekuzi. Upekuzi huu wa maktabani ulihusisha kutalii, kusoma kwa kina na kuchunguza riwaya teule za Babu Alipofufuka (Mohamed, 2001) na Dunia Yao (Mohamed, 2006) ili kudondoa data zilizohitajika katika kutimiza mahitaji ya utafiti huu. Riwaya hizi ziliteuliwa kimakusdi kutokana na utajiri wake katika kubainisha dhima za wahusika jumui katika sanaa ya kimajaribio. Aidha, utafiti huu ulipekua maandishi ya awali yanayoeleza na kushadidi sababu za kuzuka kwa wahusika jumui katika machapisho, tasnifu na tafiti nyingine zinazoshughulikia dhana ya fasihi ya kimajaribio. Maarifa yaliyotokana na maandishi haya yalikuwa amilifu katika kurutubisha na kusherekesha hoja zetu. Mkabala wa uchanganuzi wa yaliyomo ulitumika kufasiri data za utafiti huu huku matokeo yakiwasilishwa kinathari.

## 4. Dhima za Wahusika Jumui katika Riwaya za Dunia Yao na Babu Alipofufuka

Katika kuwasawiri wahusika jumui ambao wanapatikana kwenye kazi za kimajaribio, waandishi hutumia mbinu za kimazingaombwe ambapo kaida za uandishi za kijadi zinakiukwa (Khamis, 2017). Ili wahusika hawa waweze kutekeleza majukumu yao yanayofungamana na umazingaombwe, wao hubuniwa jukwaa au mazingira ya kiajabuajabu. Utafiti huu umebainisha dhima za wahusika jumui wenye sifa za kijonzi ambazo zinawafanya kuwa viumbe wa kinjozi na wasio wa kihalisia na umuhimu wao katika kuiendeleza simulizi. Kutokana na mtagusano wa wahusika jumui na wahusika wengine, tumeeleza umaarufu wao, upekee wa umazingaombwe na jinsi unavyojitokeza katika riwaya teule. Katika uhalisiamazingaombwe uhusika usio wa kawaida hujengwa pale ambapo mwandishi anawatumia wahusika wa kimazingaombwe katika mazingira ya kiajabuajabu ili kuwasilisha maudhui yake. Utafiti ulibaini wahusika *Ndi* na *K* kama wahusika jumui katika riwaya zilizoteuliwa. Katika riwaya ya Dunia Yao (Mohamed, 2006), mhusika Ndi amesawiriwa kama mhusika 1 Ye na wakati mwingine kama Shaib. Pia, kuna wakati mwandishi amemsawiri Ndi akiongea na mizuka ya watu wasioonekana, Bi Mise na Joshijitu, kudhihirisha umazingaombwe. Katika riwaya ya Babu Alipofufuka (Mohamed, 2001), Mohamed amemsawiri *K* kama mhusika jumui kwani katika uhalisia anaongea na watu halisi na katika ujumui, anakuwa na uwezo wa kuongea na mzuka wa babu yake, Bi Maajuza na watu aliowadhulumu walipokuwa hai.

Zifuatazo ni dhima za wahusika Ndi na K katika riwaya teule:

### 4.1. Kielelezo cha Maporomoko ya Jamii

Maporomoko ni anguko la mkusanyiko wa vitu vingi au maji yanayotiririka kwenye mteremko mkali wenye miamba (Mdee nw, 2019). Maporomoko ya kijamii hivyo basi ina maana ya hali ya watu kushuka hadhi ya kiuuchumi na kuyeyuka kimaadili katika jamii. Mwandishi amemtumia mhusika Ndi, katika Dunia Yao (Mohamed, 2006), kuwawakilisha wananchi wengi walioporomoka kihali na mali katika jamii. Katika Dunia Yao (Mohamed, 2006), mhusika Ndi ameporomoka kihali na mali. Ananshindwa kushirikiana na watu kama ilivyokuwa hapo awali, familia na hata marafiki zake.

Kabla ya kuipoteza kazi yake, Ndi alikuwa mume aliyeitambua haki za mkewe na baba aliye ngao kwa watoto wake wote. Baada ya kufutwa kazi serikalini alikokuwa na cheo cha juu kwa tuhuma za kupigania haki za wananchi, anashindwa kuwa mfano kwa nyumba yake na kuanza tabia ya kurudi nyumbani usiku wa manane kila mtu akiwa ameshalala ili asiwaone nyusoni. Anajifungia chumbani mwake asitake kushirikiana na mtu yeyote akiamini kwamba wangetafuta njia ya kujisaidia wenyewe. Jukumu la kuwalea wanawe alimwachia Bi *M* ambaye hakuliweza kwani baadaye wanawe wanapotoka kimaadili. Kwa mfano, Yungi anajiingiza katika ukahaba na anarudi nyumbani saa tisa na nusu alfajiri akiwa amelewa. Pia, anamkosea babake Ndi heshima kwa kuzungumza naye apendavyo (uk. 25). Ndi anashindwa kuithibiti familia yake kwa sababu ya hali yake ya kukosa kazi. Anasema:

> …mtu kama mimi kuporomoka namna hii. Kwa hakika si kuporomoka tu, nimevunjikavunjika! Nimeanguka kutoka pale nilipokita katikati ya ngazi, baada ya bwana mkubwa mmoja kuja na shoka lake kuichanja sehemu ya chini ya miguu ya ngazi tuliyosimamia akina sisi. Mwanguko ulikuwa mkubwa (uk. 20).

Kupitia kwa dondoo hili mwandishi anaonesha vile ambavyo hali inaendelea kuwa mbaya siku baada ya nyingine. Anakiri kuwa yale aliyoyajua hapo awali sio anayoyaona hasa kimaadili. Ndi anaiita hali hiyo 'ndwele', ambayo wengine wanaichukulia kama wendawazimu (uk. 3). Kupitia kwa mhusika Ndi, tunaona jinsi ambavyo maporomoko ya kiuchumi yanayotokana na kupoteza ajira yanavyoweza kusababisha utepetevu wa kimajukumu, kuvunjika kwa ndoa na hata malezi mabaya kwa watoto.

Mwandishi kupitia kwa mhusika Ndi anaonesha jinsi maporomoko yanavyoweza kumfanya kila mtu katika jamii kujishughulisha na mambo yake bila kumjali mwenzake. Wakati Kilua anamweleza babake Ndi kuwa Yungi anaugua UKIMWI, Ndi haathiriki na habari hizo. Yungi anaonekana akivuta sigara mbele ya baba yake, na kutojisetiri kimavazi; ishara ya kuporomoka kwa utamaduni wa Kiafrika unaotokana na utelekezaji wa jukumu la malezi ya mzazi (uk. 104). Yungi anaishia kumkabili na kumkosoa baba yake Ndi mbele ya watu. Hii ni ishara ya kudorora kwa maadili ya Kiafrika miongoni mwa vijana na dalili za kizazi kijacho kilichoporomoka kimaadili.

### 4.2. Kielelezo cha Ukengeushi

Kwa mujibu wa Abdallah (2021), ukengeushi una maana ya kujitenga na utamaduni unaojulikana au kubanduka kutoka kwa hali iliyozoeleka na kuanza kujihusisha na mambo ya kigeni. Katika Dunia Yao (Mohamed, 2006), mwandishi anaona mabadiliko katika dini; tofauti na ilivyokuwa kabla ya wakati huu. Anaamini kuwa dini inafaa kupigana na utandawazi, jambo ambalo halifanyiki. Anaonesha maovu yaliyo katika dini yanayosababisha mabadiliko hasi na kuafikiana na Althusser (1968) kuwa dini ni mojawapo tu ya asasi za kiutawala na wala haisaidii katika kukuza maadili. Anasema:

> Na naona kuwepo kwa dini mpya ambayo imeundwa na viji-ungu kama vile sayansi, teknolojia na utashi wa pesa (uk. 135).

Katika dondoo hili, mwandishi anaona vipashio vya utandawazi, hasa sayansi na teknolojia sawa na vijiungu vinavyoabudiwa katika dini mpya iliyozuka. Ann (2013), aliona kuwa, uvumbuzi wa kiteknolojia umechangia mabadiliko mengi katika jamii. Maoni haya yanashabihiana na ya Ndi anayesema kuwa utandawazi umesababisha mabadiliko hasi kwenye sehemu nyingi zikiwemo shuleni na nyumbani. Mohamed anaonesha jinsi ambavyo nchi zilizostawi zinavyozipiganisha mataifa yanayoendelea kupitia kwa utandawazi. Anasema nchi za Kusini na Mashariki zinapoendelea kuzozana, zinadidimia huku nchi zilizoendelea zikiendelea kustawi. Mwanya kati ya nchi hizi huzidi kuongezeka (uk. 212).

Kwa mujibu wa mwandishi, matatizo yanayosababishwa na utandawazi ni mengi yakilinganishwa na faida zake na hivyo haufai kwa mataifa machanga. Anasema kuwa, utandawazi ni njia ya kibepari na kikoloni ambayo mataifa yaliyostawi yanatumia kuendeleza dhuluma dhidi ya mataifa duni. Pia, wanatumia mfumo huo kujiendeleza huku mataifa machanga yakiendelea kuzama kwenye ulitima. Katika riwaya ya Babu Alipofufuka (Mohamed, 2001), mhusika K katika kasri lake la kifahari anafuga mbwa wake anayejulikana kama "Doggy." Katika mandhari ya kihalisia, Biye, mtumishi wa pale nyumbani ana wajibu wa kuhakikisha mbwa huyo amekula kila jioni. Matukio ya kustaajabisha yanafanyika katika kasri la K kwani katika umazingaombwe, babu Mzuka anaenda chumbani mwa "Doggy" na kukichukua chakula anachopelekewa bila yeyote kumwona. Kitendo hiki amekifanya zaidi ya mwezi mmoja. Sababu za kuchukua chakula hicho, Mzuka anasema ni kuwapa majirani ambao hawana chakula. Kulingana naye, si hekima binadamu kulala njaa huku mbwa akila chakula kizuri. Anasema kuwa hata wakati wao mbwa walilishwa kwa mabaki baada ya watu kushiba (uk. 2).

Kwa vile K haelewi kinachoendelea, anawalaumu watumishi wake akidhani ndio wanaochukua chakula cha Doggy. Jambo hili linamfanya awafute kazi wafanyakazi wakati wote. Ila hili haliwi suluhisho kwa sababu Mzuka anaendelea na tabia yake ya kuondoa chakula. Cooper (1998) na Wamitila (2003) wanasema, Uhalisia

mazingaombwe hueleza na kuwasilisha matukio ya kiajabu, ya kichawi na yasiyoaminika. Haya yanaamilisha mhimili wa nadharia ya Uhalisiamazingaombwe unaohoji kuwa wahusika huathiriwa na nguvu ambazo hawaelewi wala kuweza kuzidhibiti; yaani nguvu zinazozidi nguvu za wanadamu wa kawaida na ambazo hawana msukumo wa kujinasua nazo katika kubainisha mambo yanayofanyika kihalisia katika jamii.

Akiwa kule Neo-Casino, K anaagiza vyakula vya mawazoni, visivyo vya utamaduni wake. Anaagiza samaki wabichi, nyama ya kobe, nyama mbichi ya nguruwe, kondoo na ng'ombe iliyorowekwa katika damu mbichi. Vinaliwa kana kwamba unalazimishwa kumeza. K na viongozi wenzake wametumiwa kuonesha jinsi ambavyo viongozi wengi walivyokengeushwa na utamaduni mpya. Mzuka anamweleza K kuwa:

> …mtu akiwa na uwezo, anaweza kukigeuza kitu chochote kibaya kuwa kizuri na dunia nzima itamwitikia hewalla na tena kumfuata kuhalalisha visivyohalalishika (uk. 38-45).

Dondoo hilo linaashiria uwezo walionao viongozi wa kubadilisha maadili kwa kuwafanya watu wafuate yasiyokubalika kimaadili. Mohamed analikashifu tendo hilo kwani badala yake, viongozi wanafaa kutumia ushawishi wao kukuza maadili miongoni mwa wananchi.

K anaagiza vyakula visivyostahili kuliwa hasa katika utamaduni wa Kiafrika. Vyakula hivyo ni kama vile chatu wa kutokosa, nyoka wa kukausha, kijibwa kilichochomwa, nyangumi aliyekaangwa, beetles na hata mende. Anamdharau mwanamke aliyeketi naye eti ni wa tabaka la chini na wala si wa kiwango chake kwa kukataa kuvila vyakula vile ilhali hata yeye anafahamu vyema kuwa vyakula hivyo havistahili kuliwa, hasa katika utamaduni wa Kiafrika. Na anasisitiza kuwa, 'leo litakula visivyolika litake lisitake.' (Kur. 36-37).

Klabu atakayo kuanzisha K pamoja na marafiki zake wa kigeni kwa jina la FKK litakuwa la kujifurahishia katika usherati. Asichofahamu K anapokubaliana na wazo la ujenzi wa mradi huu ni kuwa ana watoto ambao huenda wakanaswa na mtego huu. Kidawa binti K hatimaye anaonekana akifanya usherati katika klabu hii. K anaathiriwa na nguvu ambazo haelewi wala kuweza kudhibiti pale ambapo Mzuka, mhusika asiye wa kihalisia, anamzuru na kumwambia kuwa akiupuuza ushauri wake, vitukuu na vining'ina wake wataathirika na matendo yake na hatimaye kuhukumiwa (kur. 42-45).

Mwandishi anatueleza kuwa *K* amejenga kasri kubwa sana linalofananishwa na kasri la Dracula kwa mujibu wa marafiki zake Miyawaza, Di Livio, Delpiero na Von Heim. Bawa moja la kasri lilipiga hatua kushoto na kupaa angani. Bawa jengine lilikata mbuga kulia na kunong'ona na hewa za huko. Kisha linajitokeza nje kwa mkao wa bi nene linalotoa fua mbele. Kila bawa linajitosheleza kwa maskani kamili na meko yake na kumbi zake na misala yake na mabafu yake na mahamu yake na varanda yake. Vyumba vyake visivyo idadi vinajitahidi kwenda juu kama vile jumba la makomanzi. Pia, K anaagiza miti, mimea na maua maksudi kutoka nchi za mbali kuja kuijamili fahari yake ilhali mimea hiyo inaweza kupatikana humo nchini (kur. 15-16). *K* anadhihirisha ukengeushi kwani mambo anayoyafanya yanatofautiana pakubwa na mila na desturi za Kiafrika. Anaona kuwa kila kilicho kizuri hutokana na uzunguni.

### 4.3. Kielelezo cha Umma Uliodhulumiwa

Kwa mujibu wa Mdee nw (khj), dhuluma ni kitendo cha kumnyima mtu haki au stahiki yake au uonevu. Kiptum (2017) anasema, dhuluma ni kumnyanyasa au kumnyima mtu haki yake. Hivyo basi umma uliodhulumiwa ni wananchi walionyanyaswa kwa kunyimwa haki au stahiki yao au kuonewa. Katika riwaya ya Dunia Yao (Mohamed, 2006), mhusika Ndi anatuonesha namna ambavyo wananchi wa tabaka la chini wanavyodhulumiwa. Viongozi wanapora mali ya umma na kuwaacha wananchi katika ulitima. Wanawafanyia maamuzi na kuwashurutisha kutekeleza mambo wanavyopenda wao. Kupitia ubinafsi wao, wanataka wainuliwe kiasi cha kuabudiwa. Kupitia kwa Ndi Mohamed anasema:

> Wamechukua kila kitu! Wao wamekuwa ndio wafikiri wetu. Wasemaji wetu. Watendaji wetu. Wanaoishi kwa ajili yetu. Waona njaa na kiu zetu. Walimu, madaktari, wanafalsafa, wanauchumi, mashehe, mapadri na walinzi wetu. Kwa jumla waendesha maisha yetu yote… Hatutarajiwi kusema. Hatutarajiwi kushiriki hata mambo yanayohusu nafsi yetu… (uk. 43).

Maelezo hayo yanaashiria kuwa Afrika bado haijapata uhuru. Kwamba japo wakoloni hawapo, ukoloni mamboleo unashuhudiwa kupitia kwa viongozi wakatili. Viongozi hawa wanaendeleza dhuluma, ukandamizaji na usaliti katika mataifa yao dhidi ya wanyonge kwa kutwaa na kumiliki nyenzo zote za uchumi, ulinzi na imani. Wananchi wamegeuzwa vipofu wasiojijua, mbumbumbu wasiojitambua na viumbe wasiokuwa na hisia wala njaa. Kiptum (khj) anasema kuwa dhuluma na usaliti kurudisha nyuma maendeleo ya kiuchumi na kusababisha maafa.

Kupitia kwa elimu, jamii hufahamishwa haki zao na hivyo kuweza kufanya maamuzi mema maishani. Wao huwa na uwezo wa kujikomboa na kujitegemea kimawazo anavyodai Meyer (1977). Katika Dunia Yao (Mohamed, 2006), mwandishi anatueleza kuwa elimu sio tena kigezo kinachotumiwa kupata ajira. Japo vijana wanafuzu vizuri shuleni, wanadhulumiwa kwa kutoajiriwa kama anavyosema Ndi:

> Baada ya mageuzi, kazi za ngazi za juu zilitengwa kwa wastahiki fulani na wala hazikutegemea kuwa na elimu, akili au busara. Muhimu zaidi wewe ulikuwa nani, mtoto au mjukuu wa bwana gani na kama unaitikia 'ndiyo' kila wakati (uk. 16).

Taifa linalochukua mkondo wa uongozi ambao kwao ajira hutolewa kwa upendeleo ni taifa linaloelekea kuporomoka. Hii ni kwa sababu watu waliosoma na kupata ujuzi wa kufanya kazi na kumiliki maarifa ya uongozi hunyimwa nafasi. Kulingana na Ndi, hata baada ya kuhitimu na kupata ujuzi wa kutosha, ajira hutolewa

kwa wale ambao wana uhusiano na watu tajika katika jamii. Hivyo taifa linaloongozwa na viongozi wasiohitimu halifaulu kiuchumi wala kunyooka kimaadili. Katika mataifa haya, ubinafsi na ufisadi hushamiri. Ni kutokana na uongozi kama huu ndipo mataifa mengi hasa ya bara la Afrika yamesalia nyuma kiuchumi.

### 4.4. Kielelezo cha Viongozi Wabinafsi na Wafisadi

Ubinafsi ni tabia ya mtu kujali maslahi yake mwenyewe na kupuuza ya wengine (Mdee nw, 2019). Ufisadi nao ni utumiaji mbaya wa mali ya shirika au serikali. Pia ni tabia ya ubadhirifu (Mdee nw, 2019). Muthui (2019) anasema, ufisadi ni matumizi mabaya ya mamlaka kwa kujifaidi au kuwafaidi wengine. Kwa hiyo, viongozi wabinafsi na wafisadi huyajali maslahi yao wenyewe huku wakitumia vibaya mamlaka ili kujinufaisha. Naye Munyasya (2017) anaeleza kuwa, utawala mbaya huenda sambamba na ufisadi na kwamba wananchi wakiwachagua viongozi wabaya, bila shaka kutakuwa na ufisadi.

Katika riwaya ya Babu Alipofufuka (Mohamed, 2001), mwandishi anatuonesha kasri la K linaloashiria hali ya kujitakia makuu. Kasri hilo ni la kinjozi na linafananishwa na Drakula wanavyosema marafiki wa K. Lina vyumba vingi mle ndani ambavyo havitumiwi vyote. Lina uziada uliopinda na mseto wa vitu kama anavyosema D'Haen (2005). Mohamed amelitumia jengo hilo kuonesha kiwango cha ubinafsi na ufisadi walio nao watawala. Anawakashifu viongozi wa aina hii kwa sababu wanawasababisha wananchi kuendelea kuzama katika uchochole na kuishi katika mazingira duni. Kwa mshangao, babu Mzuka anamwuliza kining'ina chake K sababu ya mtu kuwa na nyumba kubwa kiasi kile, wakati akijaaliwa na Mola huweza kuishi tariban miaka tisini tu. Mohamed anasema:

Baadhi ya marafiki zake lakini hasa Delpiero, Von Heim, Di Livio na Miyazawa, walilikejeli waziwazi jumba hilo na kumwambia lilikuwa kasri la Dracula (uk. 15).

Ukubwa wa kasri unadhihirisha uroho, uhiana na ulafi wa watawala wa kuona raha katika kuhodhi mali nyingi hata wasiyohitaji. Ndani ya kasri kuna wafanyikazi tofautitofauti: walinzi, madereva, wapishi, makarani na wasafishaji. Idadi yao ni kubwa kiasi cha kumtatiza K kuwatambua. Yeye hulazimika kuitumia kompyuta wakati anapomhitaji mmoja wao (uk. 16). Mohamed amemtumia K kama ishara ya viongozi ambao wanamiliki mali nyingi kupita kiasi wanahitaji. Ni tabia ambayo anaikashifu kwani anasema hata marafiki zake wanalikejeli kasri hilo kwa kuliita 'Dracula.'

Wakati K anapata barua kutoka kampuni ya Kijerumani aliyotiliana nayo saini kuhusu kuanzishwa mradi wa FKK ikimwarifu kuwa shughuli za ujenzi wa kijiji kizima inatazamiwa kuanza mara moja, hivyo afanye haraka kutafuta pahala panapofaa, shuruti za kutafuta pahala hapo zilianzishwa (uk. 75). K anatumia mamlaka aliyonayo vibaya kwa kuwashurutisha watu kuhama kwenye mashamba yao ili apate nafasi ya kujenga mradi wake. Tabia hii inadhihirisha ubinafsi alionao K kwa sababu anaujali mradi ambao utampa pesa nyingi kuliko maisha ya wananchi ambao wataachwa bila makao kwa sababu ya kufurushwa kutoka kwa mashamba yao. Muthui (2019) anasema, viongozi hutumia vitisho na kuwanyang'anya watu mali zao.

Katika umazingaombwe, K anaathiriwa na nguvu asizoelewa wala kuweza kuzidhibiti, yaani nguvu zinazozidi nguvu za wanadamu wa kawaida. Hivyo, Mohamed anamtumia kuonesha ufisadi unaopatikana katika barabara zetu. Anapopitishwa katika miji tofautitofauti, tunaoneshwa polisi wa trafiki wanavyopokea hongo pasi na kufanya kazi yao inavyostahili. Mwandishi anasema, punde gari aina ya matwana kongwe mno liliwasili na aliliabiri kuelekea Ncha. Wakiwa safarini, abiria mmoja mwenye ujasiri na ambaye muda wote alikuwa akimkagua K alimweleza yale wanayoyapitia kama wananchi. Anamweleza jinsi ambavyo udhia wa hongo umetapakaa kotekote: vijijini, mitaani, barabarani, njiani na hata ofisini. Hii ni baada ya kupitia mateso mengi mikononi mwa polisi wa trafiki. Baadhi ya wasafiri hawafurahishwi na abiria huyu kwani wanamwona kama aliyemkosea heshima kiongozi. Hii inaonesha jinsi ambavyo watawaliwa wamedhalilishwa kiasi cha kuathirika kiakili hadi kutoweza kujiamini. Mwandishi anaeleza kuwa gari lilipofika Ncha, ugomvi tayari ulikuwa umesharipuka na watu waliokuwa sokoni wakagawika mapande walipoisikia kadhia yenyewe (kur.133-137).

### 4.5. Zana ya Kuyakinisha Umazingaombwe

Roh (1925) anasema kuwa umazingaombwe ni mtindo unaotumiwa na waandishi wa fasihi kuyaeleza mawazo yao huku wakifichua na kubainisha miujiza iliyomo katika maisha ya kawaida. Katika riwaya ya Dunia Yao (Mohamed, 2006), wakiwa katika safari iliyoandaliwa na Wajerumani ya kuwawezesha vijana wa dunia kufahamiana usiku wa manane kule bandarini, Naima ambaye ni mhusika wa kimazingaombwe anamtokea Ndi. Ndi anaathiriwa na nguvu asizoelewa wala kuweza kuzidhibiti; yaani nguvu zinazozidi nguvu za wanadamu wa kawaida. Hivyo anashindwa kujinasua. Baadaye Naima anajitambulisha kwake kama kivuli anayejaribu kurudi katika ufu baada ya kuishi hapo zamani (uk. 97). Nukunya (1992) anasema, mwanadamu anapokufa, mwili ndio huharibika lakini nafsi yake huenda dunia nyingine kuliko na roho za wafu wengine. Anasema kuwa kifo si mwisho wa maisha ya mwanadamu kwani katika dunia ya kiroho, wafu huwa na nguvu za kuwatawala binadamu hai hasa kwa kuwaadhibu wanaotenda maovu huku wakiwahongera wenye maadili.

Katika umazingaombwe, Ndi huzungumza na nafsi yake mara nyingi. Anakiri kuchoka kusema ndani kwa ndani na nafsi yake. Bi Mize, kiumbe cha kisaasili, anavyombainisha Abrams (1971), anamwambia aseme naye. Ndi anashangazwa na maneno hayo kwani anamwelewa Mize kama kivuli na kwa hivyo hawawezi kuzungumza. Ndi anamwambia kuwa angetaka kujua kwa nini kila akisimama huja jini kumpiga rungu la kichwa au kimbunga kumsukasuka na kumwangusha chini (uk. 74). Haya ni matukio ya kimazingaombwe kwani yanafanyika tu mawazoni mwa Ndi. Freud (1965) na Farady (1972)

wanasema kuwa umazingaombwe hujitokeza wakati mhusika anapokuwa na nafsi mbili; tulivu na inayotembea kimiujiza ndotoni.

Katika Babu Alipofufuka (Mohamed, 2001), K anashangazwa na matukio ya kimazingaombwe yanayofanyika wakiwa safarini kuelekea Neo-Casino. Garini mwake, ghafla kioo kinajitokeza na kumtenganisha na dereva wake Mzula. Baadaye, milango ya gari inafunguka wakati gari likienda bila utaratibu maalum. Wakati huohuo, K anamwona dereva wake akiwa amebadilika na kuwa nyani na kuketi kama popo huku akiliendesha gari kwa kutumia miguu yake ya nyuma (kur.18-20). Kenduiywa (2022) anasema kuwa umajaribio hujengwa pale mandhari halisi hugeuzwa kuwa ya kinjozi.

Babu Mzuka anamwandama K kila mahali anakoenda tangu aingie maishani mwake. Anamsababishia shida baada ya nyingine kiasi cha kumkosesha amani. K anaathiriwa na nguvu asizoelewa wala kuweza kuzidhibiti; yaani nguvu zinazozidi nguvu za wanadamu wa kawaida. Hivyo hana uwezo wa kujinasua. Mzuka anamsihi K abadilishe tabia yake ili aepuke hukumu inayomsubiri. Anamwambia kuwa maisha yake yamebadilika kwa vile amekuja karibu naye na ataishi pamoja naye ili amsaidie kutatua shida zake (kur. 21-23). Lakini, K hasikii. Ametumiwa kama kielelezo cha viongozi wenye kiburi na mapuuza.

Alipofika ofisini mwake, K alipigwa na bumbuazi kwani anapoingia ndani, anakutana na watu wengi wenye mikono mine katika viungo vyao vyote vya mwili; magotini, viunoni na masikioni. K anawaona viumbe wale wakiharibu vitu pale ofisini na walinzi wanajaribu sana kuwazuia kuendeleza uharibifu huo ila viumbe wale wanabadilika na kuwa moshi baadaye wanapotea machoni mwao. Tukio lile linawaacha na mahangaiko mengi na mioyo iliyovunjika (kur. 68-69). Mwandishi anawatumia viumbe hao wa kimazingaomwe kutekeleza majukumu ya kihalisia kama binadamu wa kawaida (Hegerfeldt, 2005).

### 4.6. Kielelezo cha Viongozi wenye Mapuuza

Kulingana na Mdee nw (2019), kupuuza ni kutotia maanani au kudharau. Kwa hivyo kiongozi mwenye mapuuza ni yule ambaye hatilii maanani ushauri au mwenye kudharau ushauri wa wengine. Wanajamii hutegemeana, mmoja na mwingine. Mtu akiwa pekee yake hawezi kujitosheleza, hivyo kila mtu anamhitaji mwenzake (Njogu na Chimerah, 2011). Katika riwaya ya Babu Alipofufuka (Mohamed, 2001), wakitoka Neo Casino, babu Mzuka anamwonya K dhidi ya maovu anayoyafanya na kwamba lazima ataadhibiwa kwa makosa hayo yote lakini K anaupuuza ushauri huo. Mzuka anamfahamisha kuwa tabia yake ovu ndiyo inamsababishia matukio ya kiajabu ili ashtuke na kubadilika. Lakini K hazingatii ushauri wa babu Mzuka. Kwa mujibu wa Curzer (1996), ushauri humjulisha mtu kuhusu mambo yanayokubalika na yasiyokubalika kulingana na hali na wakati.

Kutokana na maneno ya babu Mzuka, mwandishi anasema kuwa K hakuweza kubaini iwapo alikuwa macho au njozini. Alikuwa ameathiriwa na nguvu asizoelewa wala kuweza kuzidhibiti; yaani nguvu zilizozidi nguvu za wanadamu wa kawaida na hivyo kushindwa kujinasua. K hakujali wala kurekebisha tabia yake hata kidogo. Huko barabarani, magari yaliendeshwa polepole isifahamike aliyekuwa na idhini ya kupita au aliyefaa kumpisha mwenzake. Waliotembea kwa miguu pia walikuwa mashakani.

Katika mazingira hayo ya barabarani, K na dereva wake Mzula, wanakumbana na mchanganyiko wa matukio. Watoto wa kuombaomba wanatokea na kulizunguka limonsin huku wakiomba angalau thumni. Hapohapo, vijana waliokuwa na ghadhabu, hasira iliyoonekana machoni mwao mlimojaa wekundu wa moto wa makaa, walifinyanga ngumi na kuligonga gari kwa ghasia. Wakati uleule, walichipuka vimada waliojisetiri kwa minisketi wakitembea taratibu na kwa maringo karibu na limonsin huku wakimwashiria K nia ya kutaka kushiriki mapenzi naye. Mandhari haya yanaonesha kiwango cha ulitima walimo ndani wananchi huku viongozi kama K wakiwapuuza. Baadaye, wananchi wanaamua kuchukua sheria mikononi mwao na kufanya chochote wanachodhani kitaweza kuwakomboa.

Katika safari yao kuelekea dunia mpya, babu Mzuka anamwambia K avue miwani yake ya jua ili avae figu ambalo ni sawa na miwani katika dunia hiyo. Japo ilikuwa muhali kwa K kuitoa miwani yake ya jua, hakuwa na budi ila kutii maagizo kwani aliathiriwa na nguvu asizoelewa wala kuweza kuzidhibiti, nguvu zilizomzidi. Njiani, walikutana na wananchi ambao walinung'unika kuhusu utawala mbaya wa viongozi wao akiwemo K. Walipitapita mbele ya gari la K wakiongea lakini hawakuwaona, baadaye walitoweka.

Mzuka anamweleza K kuwa dunia zao zinapakana kiasi kwamba wakisema, wanawasikia ila hawawasikilizi (kur. 88-99). Mohamed amemtumia K kuashiria tabia ya baadhi ya viongozi ya kutosikiza vilio vya wananchi waliowachagua uongozini. Hawakumbatii na kutumia ushauri vyema ili kusababisha mabadiliko chanya yanayoleta usalama na yanayokubalika na wanajamii kama anavyosema Jonas (2017). Punde wanapopata vyeo, huyaziba masikio yao wala wasijihusishe na mahitaji ya wananchi. Mwandishi analikashifu tendo hili. Anatumia hadithi ya ngamia na msafiri jangwani kueleza tabia ya K ya kukosa shukrani baada ya kusaidiwa alipokuwa katika shida. Anasema:

> Niruhusu nitie kichwa tu, haya! Msafiri anakubali. Niruhusu niingize shingo tu, vyema! Msafiri anamwitikia. Niruhusu nitie kifua tu, sawa! Msafiri anamkubalia. Niruhusu niingize miguu tu, hewalla! Msafiri aridhika. Niruhusu nitie mkia tu, ndiyo! Lo! Kahamanika msafiri, kapigwa teke na kasalia kula baridi nje ya hema (kur. 98-99).

Kutokana na simulizi hili, Mohamed anatuonesha utovu wa shukrani kwa baadhi ya watu kama alivyofanya K. Analikashifu tendo hilo kwani anaamini kuwa binadamu yeyote akishafanyiwa wema anapaswa kusema

asante. Hili ni jambo la msingi lakini linaonekana kupuuzwa na watu wengi ambao baada ya kusaidiwa, huwasahau waliowapa msaada na hata wakati mwingine kuwadhalilisha bila kukumbuka kuwa huenda wakawahitaji siku nyingine. Badala ya K kuonesha shukrani kwa Sururu baada ya kusaidiwa, anamnyang'anya mkewe Zuhura Mapozi.

### 4.7. Zana ya Kutekelezea Hukumu

Hukumu ni uamuzi ambao hutolewa na hakimu katika kumaliza kesi (Mdee nw, 2019). Katika Babu Alipofufuka (Mohamed, 2001), babu Mzuka anamwambia K kuwa watakapokuwa wakirudi watapitia baharini, waliko mahakimu wa wakati. Wao ndio watakaosikiza na kuamua kesi zinazomkabili K. Mzuka anamwambia K kuwa ameshtakiwa na wakati, aliowakosea na hata yeye mwenyewe. Babu Mzuka anamwambia K kuwa hana hiari, lazima ahukumiwe. Wakati ukifika, hatakuwa na budi ila kutii amri. Anamwambia kuwa hata akifa, watoto wake, jamaa zake hata kivuli chake kwa namna yoyote ile itahukumiwa. Matukio hayo yanashadidia maoni ya Chanady (khj) anayesema kuwa uhalisiamazingaombwe unahusu matukio yasiyo ya kawaida. Mwandishi anamtumia K akiwa mahakamani kudhihirisha kuwa hakuna kiongozi yeyote mwovu, asiyewajibika kwa jamii na anayekosa kufanya kazi yake kwa uadilifu ataepuka hukumu (kur. 137-143).

K anaporudi uhalisini anapata kuwa yeye ni mtu wa kawaida kwani alikuwa amefutwa kazi na kuondolewa watumishi pamoja na walinzi wake wote. Nyumbani kwake hakukuwa na maji wala nguvu za umeme. Alikimbilia Neo-Casino ili kutafuta msaada ila hakuupata. Hali hiyo inamfanya aikumbuke familia yake; mkewe Kikuba pamoja na wanawe, Kidawa na Bamkubwa ambao mwandishi anasema walishabadilika na kuwa wehu kwa sababu ya hali ngumu ya maisha waliopitia baada ya kupuuzwa na K kwa miaka mingi alipokuwa mamlakani. Mambo haya yote yanampa K msongo wa mawazo asijue la kufanya. Baadaye anaamua kujitia kitanzi. Akiwa mfu anateremka ahera kisha baadaye anajaribu kurudi ulimwenguni kama pepo ili aonane na wanawe lakini hafanikiwi.

Alitamani apate nafasi ya kuwaomba msamaha lakini alikuwa amechelewa. Mohamed anatumia maelezo hayo kumjulisha msomaji kuwa kila kitu kina wakati wake na ukishapita, huenda isiwe rahisi kurekebishwa. Amemtumia K kama kiongozi jeuri ambaye hata baada ya babu Mzuka kujaribu kumwadhibu na kumwonesha njia bora ya kufuata, habadilishi tabia yake. Hivyo anakumbana na hukumu ambayo kamwe binadamu yeyote mwovu hawezi kuepuka (kur. 148-168).

## 5. Hitimisho

Wahusika katika fasihi za kimazingaombwe wanaumbwa kwa lengo la kuwafanya wawe na masimulizi yenye mwambatano wa kina na wanatekeleza majukumu yao vilivyo ili watambulike wazi kama wahusika jumui. Makala haya yamebainisha dhima za wahusika jumui kama ifuatavyo: kielelezo cha maporomoko ya jamii, kielelezo cha ukengeushi, kielelezo cha umma uliodhulumiwa, kielelezo cha viongozi wabinafsi na wafisadi, zana ya kutekelezea umazingaombwe, kielelezo cha viongozi wenye mapuuza na kama zana ya kutekelezea hukumu. Wahusika hao wameweza kuafiki majukumu yanayoambatana na mahitaji ya sanaa za kisasa na uchunguzi wa masuala ya kijamii kwa mtazamo wa Kiafrika. Utafiti huu umebainisha nafasi ya malighafi asili za Kiafrika, yaani umazingaombwe unaochukua sura ya uchawi kusuluhisha matatizo yanayoletwa na maendeleo ya sayansi pamoja na utandawazi. Kadhalika, dhima zilizobainishwa katika makala haya, zimechangia katika kuleta uelewa mpana wa nafasi ya mhusika jumui katika riwaya ya Kiswahili ya kimajaribio.

## Marejeleo


Abrams, M. H. (1971). The mirror and the lamp: Romantic theory and the critical tradition, 360. New York: Oxford University Press.

Althusser, L. (1968). Reading capital. Paris: Librairie Francois Maspero.

Ann, S. S. (2013). Usasa na mwanamke wa kisasa katika Nyuso za Mwanamke ya Said Ahmed Mohamed (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Cooper, B. (1998). Magical realism in West African fiction. New York: Routledge.

Curzer, H. J. (1996). Aristotle's Bad Advice about Becoming Good. Philosophy, 71(275), 139- 146.

D'Haen, T. L. (2005). Magical realism and postmodernism: Decentering privileged centers. Journal of Language, Literature and Popular Culture, 2(1).

Farady, A. (1972). Dream power. London: Hodder and Stoughton.

Freud, S. (1965). The interpretation of dreams, stachey, J. Trans. Newyork: Avon.

Green, J. A. (2009). Dreams of freedom: Magic realism and visionary materialism in Okri and Blake. Romantism, 15 (1), 18 -32.

Hegerfeld, A. (2005). Contentious contributions: Magical realism goes British. Journal of Interdisciplinary Studies in Literature, Continental Philosophy, Phenomenological Psychology, and the Arts, 5(2), 62-86.

Jonas, M. (2017). Resentment of advice and norms of advice. Ethical theory and moral practice. JSTOR, 20(4), 813-828.

Kenduiywa, A. C. (2022). Uwasilishaji wa wahusika na uhusika wa kimazingaombwe katika riwaya za Watu wa Gehenna na Babu Alipofufuka (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Kabianga.

Khamis, S. A. M. (2017). Vionjo vya riwaya mpya ya Kiswahili. Kioo cha Lugha, 5(1),13-23.

Kiptum, J. T. (2017). Uyakinifu wa maudhui makuu katika utenzi wa Abdirrahman na Sufiyani (Tasnifu ya uzamifu). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Lee, G. (2004). A million little choices: The ABCs of CNF. London: Yale University Press.

Mbatia, M. (2002). Kamusi ya Kiswahili. Nairobi: Standard Text-books Graphics and Publishing.

Mdee nw. (2019). Kamusi ya Karne ya 21. Nairobi: Longhorn Publishers.

Meyer, J. W. (1977). The effects of education as an institution. American Journal of Sociology, 83(1) 55-77.

Mohamed, S. A. (2001). Babu Alipofufuka. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, S. A. (2006). Dunia Yao. Nairobi: Oxford University Press.

Mulokozi, M. M. (1996). Fasihi ya Kiswahili. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Munyasya, F. M. (2017). Mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko katika Kufa Kuzikana na Kidagaa Kimemwozea (Tasnifu ya uzamifu). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Muthui, E. K. (2019) Tathimini ya maudhui katika tamthilia teule za Kiswahili zinazotahiniwa shuleni za upili nchini Kenya: Mstahiki Meya na Kigogo (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya.

Njogu, K. & Chimerah, R. (2011). Ufundishaji wa fasihi: nadharia na mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nukunya, G. K. (1992). Tradition and change in Ghana: An introduction to sociology. Accra: Ghana University Press.

Roh, F. (1925). Magic realism: Post –expressionism: Magical realism, theory, history, community. Durham: Duke University Press.

Wamitila, K. W. (2003). Kamusi ya fasihi, istilahi na nadharia. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2010). Kanzi ya fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi. Nairobi: Vide- Muwa Publishers.

Warnes, C. (2006). Magical realism and the legacy of German idealism. The Modern Language Review, 101(2), 488–498. https://doi.org/10.2307/20466796

Zamora, L. P. (1995). The visualizing capacity of magical realism: Objects and expression in the work of Jorge Luis Borges. In L. P. Zamora, & W. B. Faris (Eds.), Magical realism: Theory, history, community. Durham: Duke University Press. pp. 21-37.